

MALEZI YA VIFARANGA

Kuku site

A: MAANDALIZI.

MAANDALIZI

1. Andaa banda/chumba (brooder room) utakachokitumia kwa ajili ya kuleavifaranga kiwe na sifa zifuatazo:



- Hewa ya kutosha.
- Mwanga wa kutosha
- Chanzo cha joto kama vyungu vya joto au bulb zinazozalisha joto.
- Mazingira rahisi ya kufanya usafi.
- Nafasi ya kutosha kuepusha msongamano wa vifaranga.



2. Andaa vifaa vitakavyotumika kuwashudumia kuku kama:

- Vyombo nya maji (Drinker)
- Vyombo maalumu nya kuwekea chakula (feeder)
- Vifaa nya kufanya usafi kama koleo, mifagio n.k



3. Andaa chakula kwa ajili ya viafaranga ,Multivitamins na dawa kwa ajili ya huduma ya kwanza endapo kuna changamoto itajitokeza.



B: MAMBO YA KUZINGATIA WAKATI WA MALEZI YA VIFARANGA.

1. USAFI wa banda, Vyombo nya maji na vyombo nya chakula. (Uchafu ndiyo chanzo cha kuenea na kuzaliana kwa vimelea vinavyosababisha magonjwa) .



kuku.great-site.net

2. Chakula bora cha vifaranga (Vifaranga wa nyama/ Vifaranga wa kwa ajili ya mayai) Chenye virutubisho vyote vinayvohitajika. Vifaranga waandaliwe chakula BORA na wapewe Kwa wakati kipimo kinachowatosha kulingana na rika lao.



kuku.great-site.net

3. Vifaranga wanahitaji MULTIVITAMIN (Vitamini) ambayo mara nyingi huwekewa katika maji ya kunywa ili kuwafanya wawe na afya bora na kuwakinga na magonjwa.



4. Joto la banda(chumba cha vifaranga/brooder room) lisizidi nyuzijoto 35oC na lisipunguae 24oC wiki nne za mwanzo.



5. Vifaranga wanahitaji usalama wasishambuliwe na wanyama wakali au kitu chochote cha kuwadhuru. Pia wasichanganywe na kuku wengine wakubwa.
6. Vifaranga wanahitaji uangalizi wa karibu sana kujua changamoto zinazowakabili na kuwatimizia mahitaji yao kwa wakati.



7. Vifaranga wapatiwe chanjo zote muhimu kwa wakati sahihi ili kuepusha Hasara inayoweza kuepukwa.

8. Tunza kumbukumbu za chanjo, Gharama za chakula, dawa na vifaa mbalimbali ili uweze kufanya tathimini na maboresho hapo baadae.

Imepakuliwa : 10/09/2024

Inapatikana :<https://kuku.great-site.net>